

Mbegu ya Hitilafu
Phoenix, Arizona, USA
Januari 18, 1965

1 Nimechagua usiku wa leo kwa ajili ya somo fupi, ama kusoma kwa kifupi, Bwana akipenda, kutupa muktadha wake, kutoka kwenye Mathayo Mtakatifu 13:24 hadi 30. Na halafu pia na—nataka kusoma kutoka 36 hadi 40, katika dakika chache tu. Sasa Mathayo Mtakatifu, mlango wa 13, na kuanzia kifungu cha 24 cha sura ya 13 ya Mathayo Mtakatifu. Sikilizeni kwa makini kusomwa kwa Neno. Maneno Yangu yatashindwa, bali Yake hayatashindwa.

Akawatolea mfano mwingine, akisema, Ufalme wa mbinguni umefanana na mtu aliyepanda mbegu njema katika konde lake;

Lakini watu walipolala, akaja adui yake akapanda magugu katikati ya ngano, akaenda zake.

Baadaye majani ya ngano yalipomea na kuzaa, yakaonekana na magugu.

Watumwa wa mwenye nyumba wakaenda wakamwambia, Bwana, hukupanda mbegu njema katika konde lako? Limepata wapi basi magugu?

Akawaambia, Adui ndiye aliyetenda hivi. Watumwa wakamwambia, Basi, wataka twende tukayakusanye?

Akasema, La; msije mkakusanya magugu, na kuzing'oa ngano pamoja nayo.

Viacheni vyote vikue hata wakati wa mavuno; na wakati wa mavuno nitawaambia wavunao, Yakusanyeni kwanza magugu, myafunge matita matita mkayachome; bali ngano ikusanyeni ghalani mwangu.

2 Je! Uliona, "Kusanyeni magugu kwanza, mkayafunge matita"? Sasa, nikisoma jambo hili, kulikuwa na kitu cha ajabu kilichonijia wakati nilipokuwa nimeketi juu ya Milima ya Catalina hivi majuzi usiku, katika maombi. Ndipo nikawazia, wapi ningeweza kupata neno ambalo ningeweza kutumia kwa jambo hili nililotaka kunena juu yake usiku wa leo?

Nami nikashuka nikaenda nikaona neno la hitilafu, kwa hiyo nikachukua kamusi na kuangalia maana ya neno hitilafu. Nalo linamaanisha ni "kupanda hitilafu," ama—ama, "kuwa kinyume," kama isemavyo Webster, "kupanda hitilafu, kitu cha tofauti," ama, "kuwa kinyume cha jambo ambalo limekuwako tayari." Kwa hiyo nikawaza, fungu la maneno usiku wa leo, ningeliita: Mbegu Ya hitilafu. Na tumaini kwamba Bwana atalibariki Neno Lake sasa tunapoliendea.

3 Na pia tunajua Yeye alifasiri, katika kifungu cha 36 na—na hadi 43, jinsi ambavyo uzao huu ulikomaa. Na wakati tukiwa katika jambo hilo, hebu na tusome hilo pia, kifungu cha 36 sasa hadi 43.

Kisha Yesu akawaaga makutano, akaingia nyumbani; wanafunzi wake wakamwendea, wakasema, Tufafanulie mfano wa magugu ya kondeni.

Akajibu, akasema, Azipandaye zile mbegu njema ni Mwana wa Adamu;

Lile konde ni ulimwengu; zile mbegu njema ni wana wa ufalme; na yale magugu ni wana wa yule mwovu;

Yule adui aliyeyapanda ni Ibilisi; mavuno ni mwisho wa dunia; na wale wavunao ni malaika.

Basi, kama vile magugu yakusanywavyo na kuchomwa motoni; ndivyo itakavyokuwa katika mwisho wa dunia.

Mwana wa Adamu atawatuma malaika zake, nao watakusanya kutoka katika ufalme wake machukizo yote, na hao watendao maasi,

Na kuwatupa katika tanuru ya moto, ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno.

Ndipo wenyе haki watakapong'aa kama jua katika ufalme wa Baba yao. Mwenye masikio, na asikie.

4 Huyo ni Yesu akitoa tafsiri ya mfano, Mwenyewe, kwa hiyo tunajua basi maana ya fasiri hiyo. Na sasa tunapokaribia jambo hili, hili la kupanda mbegu na—na kuvuna, sasa Yeye analifasiri. Na halafu ninaamini ya kwamba Yesu alikuwa akinena mfano huu katika siku Zake, bali alikuwa na maana ya kuwa katika mwisho wa ulimwengu, ama, mwisho wa wakati, ambao ni siku hii. Nami naamini kifungu hiki kidogo usiku wa leo kinafaa sana kwa saa tunayoishi, kwa sababu Yesu alisema dhahiri hapa ya kwamba "kukusanyika kungekuwa katika mwisho wa dunia hii," ya kwamba hapo ndipo mwisho ungekuwa; kukusanya kwa ngano, na pia kukusanya kwa magugu na kuyachoma, na kuipeleka ngano katika

Ufalme. Nami ninaamini ilikuwa hivi.

Na Andiko lingine linaniongoza kuamini hivi, nimeandika hapa chini, ni Mathayo 24:24, ambapo lilisema kwamba, likinena juu ya—kile kiti, mbega ya hitilafu. Yesu alisema ya kwamba hayo mawili yangekuwa karibu sana hata yangewapoteza walio Wateule kama yamkini. Karibu ni sawa kabisa.

5 Mahali pengine katika Maandiko ambapo imeandikwa, ambapo mvua huwanyeshea wenyehaki na wasio haki.

Ninakumbuka tukio langu la kwanza la kuja mionganoni mwa Wapentekoste. Nilikuwa Mishawaka, Indiana. Nami nilikuwa kwenye mkutano mkuu, ukumbi kama huu, ambapo Kaskazini na Kusini walikuwa wamekusanyika pamoja. Kwa sababu ya siku hizo, za ubaguzi, iliwbidi kukutana huko juu. Walikuwa ni madhehebu mawili makuu ya ndugu wa Kipentekoste. Sikuwa nimewahi kusikia habari zake wala kukutana nao hapo kabla. Mara ya kwanza nilipopata kusikia kunena kwa lugha. Na mwishoni mwa safu, ya mkutano ... Mimi nikiwa si mshiriki mionganoni mwao, nilikuwa tu kijana mhudumu wa Kibatisti, niliketi huko nyuma kabisa. Nami ninakumbuka mara ya kwanza nilipomsikia mtu ye yote akinena kwa lugha, hata sikujuu nini—yote ilikuwa ni nini. Halafu watu hawa wawili, hasa, waliketi mbele, mmoja angenena kwa lugha na huyo mwingine angefasiri yale aliyo sema huyo mwingine. Vema, nilianza tu kusoma Biblia yangu kwa nguvu niwezavyo, hapo basi, na nikaona ya kwamba hilo lilikuwa ni la Kimaandiko. Hilo ndilo hasa Maandiko, Roho Mtakatifu angefanya.

6 Vema, yapata siku moja baada ya hapo ... Usiku huo moyo wangu ulisisimka sana. Nililala kwenye shamba la mahindi. Sikuwa na fedha za kutosha kununulia ki—ki—kitanda, kwa hiyo nilikuwa tu na fedha za kutosha kuendea nyumbani, nami nikanunua donati chache, zimekaa kwa siku kadha, ama roli, viliitwa hivyo, na kwa ajili ya kiamshakinywa changu. Nami nilikaribishwa kula pamoja nao, bali sikuwa na pesa za kuchangia. Katika siku hizo, hiyo ilikuwa ni katika wakati wa kuzorota kwa uchumi, 1933, kwa hiyo mambo yalikuwa—yalikuwa ni magumu sana. Na kwa hiyo nikawaza, "Vema, nita- ... Sitaki kula pamoja nao, bali ninataka kujua walicho nacho. Wana kitu ambacho mimi sina."

Kwa hiyo asubuhi hiyo nilikuwa ... waliniuliza, "Wahudumu wote njoni jukwaani m jitambulise tu, kwamba ninyi ni nani, mnakotoka."

Vema, ni—nilisema tu, "William Branham, mwinjilisti, Jeffersonville," nikaketi chini. Vema, wakati huo nilikuwa mhudumu mchanga kuliko wote jukwaani. Na kesho yake wakanita jukwaani kuzungumza. Na halafu baada ya mimi kuzungumza, mbona, tulikuwa na wakati mzuri sana, na ndipo nikaanza kukutana na watu mbalimbali wakinialika kwenye makanisa yao. Ndipo baada ya wao ...

7 Baada ya jambo hilo, mbona, niliwazia, "Laiti ningaliweza kufikia mahali watu hawa wawili wakuu waolinena kwa lugha na kufasiri!" Hilo lilikuwa likinichoma moyoni mwangu, nililitaka sana. Vema, kama niliiyokwambia mwanzoni, karama ndogo ambayo unavuta. Unajua, karama na miito havina majuto, unavyo maishani mwako mwote, unaona, unazaliwa navyo, kama ni karama za Mungu. Kwa hiyo mimi daima, tangu nikiwa mtoto mchanga sana, daima ilinitokea, watu wanaonijua maishani mwangu mwote, wanajua hiyo ni kweli. Vema, kama niliifikiri ... Sikujuu ilikuwa ni nini wakati huo, niliita ono, sikujuu tu ilikuwa ni nini. Lakini niliwazia, "Kama ningeweza kamwe kuzungumza nao!" Vema, na roho iliyokuwa ndani ya jengo hilo ilionekana kana kwamba kweli ni Roho wa Mungu.

Kwa hiyo ni—iliinibidi kuzungumza na mmoja wao, nami nikamwuliza maswali machache, naye alikuwa Mkristo halisi kabisa. Hakukuwa na shaka juu ya jambo hilo, kwamba mtu huyo alikuwa mwamini halisi. Na mtu aliyefuata, nilipozungumza naye, kama niliwahi kukutana na mnafiki, huyo alikuwa mmoja wao. Mtu huyo kwa kweli alikuwa ... Mke wake alikuwa mwanamke mwenye nywele za shaba, naye alikuwa na watoto kwa ... watoto wawili kwa mwanamke mwenye nywele nyeusi. Ndipo nikawaza, "Vema, sasa nini? Hii hapa, mimi—mimi nimechanganyikiwa kabisa. Mimi ni mwamini wa kanuni za kimsingi; lazima liwe ni Neno, la sivyo si sahihi. Na hapa pana Roho yule, mmoja alisikika, kulingana na yote nijuayo mimi, kuwa ni halisi; na yule mwingine alikuwa hana lo lote kabisa; na Roho akiwashukia wote wawili. Sasa, hilo linawezekanaje?" Ningeninii, lilinitatiza.

8 Miaka miwili baadaye, nilikuwa nikiomba kwenye pango ambapo ningeenda kuomba. Kulikuwa na mavumbi pangoni, na alasiri moja nilitoka, nikaweka Biblia yangu juu ya gogo, na upepo ukaifungua katika Waebrania, mlango wa 6. Ambapo ilisema, ya kwamba katika siku za mwisho, jinsi ingekuwa kama tukianguka kutoka katika Kweli na kujifanya upya tena hata tukatubu, hakukuwako na dhabihu ya dhambi tena, na jinsi ambavyo miiba na michongoma, ambayo mwisho wake ni kukataliwa, ambayo mwisho wake ni kuteketezwa; lakini mvua huinyea nchi, mara nydingi, kuitia maji, kuilima; lakini miiba na michongoma ingekataliwa, bali ngano ingekusanywa. Nami nikawaza, "Vema, ni upepo tu ultokea ukafungua huo." Vema, niliweka tu Biblia chini tena. Ndipo nikawaza, "Vema, sasa nitaninii tu ..." Na hapa ukaja upepo na kuifungua. Hilo lilitukia mara tatu. Nami nikawaza, "Vema, sasa, hilo ni jambo la ajabu."

Halafu nilipokuwa nikiinuka, nikawazia, "Bwana, mbona umenifungulia Biblia hiyo nisome jambo hilo, mimi...nilipofikia mahali hapo, ambapo 'miiba na magugu, ambayo huwa karibu na kukataliwa, ambayo

mwisho wake ni kuteketezwa'?" Nikawazia, "Mbona, ungetaka kunifungulia jambo hilo pale?" Na wakati nikiangalia huko nje ...

9 Sasa, maono haya halisi huja bila kuingiza gia yoyote. Huyo ni Mungu tu. Mnaona? Nikaangalia na nikaona dunia iliyokuwa ikigeuka mbele yangu, nami nikaona yote imelimwa. Kulikuwako na mtu aliyeavaa nguo nyeupe, alizunguka-zunguka akipanda ngano. Kulikuwa kuna mtu aliyeavaa nguo nyeupe, aliyetoka akaenda akipanda ngano. Na baada ya yeze kwenda kwenye mpindiko wa dunia; akatokea mtu fulani, alioneekana wa kuchukiza, naye alikuwa ameavaa vazi jeusi, naye alikuwa akitupa mbegu za magugu juu yake kila mahali. Wote wawili wanakuja pamoja. Zote ziliota pamoja. Na zilipoota, zote zilishikwa na kiu, kwa maana mvua ilihitajika. Na kila moja ya hizo ilioneekana kana kwamba inaomba, huku imeinamisha kichwa chake kidogo, "Bwana, tipe mvua, tipe mvua." Ndipo hayo mawingu makubwa yakatokea, na mvua ikanyeshea zote mbili. Wakati ilipofanya hivyo, ile ngano ndogo iliruka juu na kuanza kusema, "Bwana asifiwe! Bwana asifiwe!" Ndipo maskini magugu hayo yakaruka moja kwa moja upande ule ule, na kusema, "Bwana asifiwe! Bwana asifiwe!"

Na ndipo lile ono likatafsiriwa. Mvua huwanyeshea wenyewe haki na wasio haki. Roho yule yule anaweza kushuka mkutanoni, na kila mtu akafurahi katika jambo hilo: wanafiki, Wakristo, na wote pamoja. Sawa kabisa. Lakini ni kitu gani? Kwa matunda yao wanajulikana. Mnaona? Hiyo ndiyo njia pekee inayoweza kujulikana.

Ndipo unaona jambo hilo sasa, kwa kuwa shayiri mwitu, ama ngano mwitu na nafaka mara nydingi huiga nafaka halisi, ya kienyeji, zinafanana sana hatia ingewapoteza walio Wateule. Nafikiri tunaishi katika wakati wenyewe, wakati mambo haya yanapaswa kuhubiriwa na kuzungumziwa.

10 Angalia katika kifungu cha 41, hizo mbili pia zinafanana sana, zinafanana sana katika siku za mwisho hata Yeye hakufanya jambo hilo... Yeye asingeweza kutegemea kanisa fulani kuwatenganisha, tuseme, Methodisti ama Baptisti, wala Wapentekoste kuwatenganisha. Yeye alisema, "Yeye huwatuma malaika Wake kuwatenganisha." Malaika anakuja kuleta utengano, ubaguzi kati ya mema na mabaya. Na hakuna mtu anayeweza kufanya jambo hilo ila Malaika wa Bwana. Yeye Ndiye atakayewaambia ni lipi ni kweli na lipi ni baya. Mungu alisema atawatuma malaika Wake katika nyakati za mwisho. Si malaika kupitia *hapa*, bali malaika wakati wa mwisho, nao wangkusanyika pamoja. Tunajua ya kwamba huu ni wakati wa mavuno unaokuja sasa. Sasa, malaika kweli anafasiriwa "mjambe." Na tunaona ya kwamba kuna malaika saba wa yale makanisa saba, na sasa ... la, katika nyakati za kanisa.

Angalia Yeye alisema ya kwamba wapanzi walikuwa ni nani, na pia ile mbegu ilikuwa ni nani. Mmoja, mpanzi alikuwa ni Yeye, Mwana wa Mungu, ambaye alitoka akaenda akipanda Mbegu. Ndipo adui akaja nyuma Yake, ambaye alikuwa ni ibilisi, na akapanda mbegu ya hitilafu, nyuma ya kupanda Mbegu ilio sahihi. Sasa, enyi marafiki, hilo limetukia katika kila wakati tangu tumekuwa na ulimwengu. Kweli kabisa. Kote tangu mwanzo, lilianza jambo lile lile.

11 Sasa Yeye alisema, "Uzao wa Mungu, Neno la Mungu." Yesu alisema, mahali fulani, ya kwamba "Neno ni Mbegu." Na kila mbegu itazaa kwa jinsi yake. Na sasa kama Mkristo, watoto wa Mungu, watoto wa Ufalme wamekuwa Mbegu ya Mungu, basi hawana budi kuwa ni Neno la Mungu, Neno la Mungu lililodhahirishwa katika wakati wanaoishi, kwa ajili ya ahadi iliyoahidiwa, Mbegu ya wakati huo. Mungu alitoa Neno Lake hapo mwanzo, na kila wakati umekuwa na Uzao wake, wakati wake, ahadi zake.

Sasa, wakati Nuhu alipojitokeza, naye alikuwa ni Uzao wa Mungu, Neno la Mungu kwa wakati huo.

Wakati Musa alipokuja, asingeweza kuja na ujumbe wa Nuhu, haungefaa kitu, kwa sababu yeye alikuwa Uzao wa Mungu wakati huo.

Ndipo Kristo alipokuja, Yeye hangekuja pamoja na wakati wa Nuhu wala wa Musa; ilikuwa ni wakati Wake, kwa bikira kuchukua mimba na kumzaa Mwana, Naye angekuwa Masihi.

12 Sasa, tumeishi kupitia wakati wa Luther, wakati wa Wesley (wakati wa Methodisti), kote katika nyakati, na wakati wa Pentekoste, na kila wakati umepewa ahadi ya Neno. Nao watu wa wakati huo, wanaodhahirishwa hilo Neno lililoahidiwa, ni Uzao wa wakati huo, kulingana na yale Yesu aliyosema papa hapa, "Wao ni wana wa Ufalme." Hiyo ni kweli. Dhihirisho la Roho Mtakatifu akifanya kazi kupitia kwa watoto Wake ni ile Mbegu ya Ufalme katika wakati huo.

Angalia, magugu yalikuwa ni yale, yule adui, Shetani, ambaye alipanda ugomvi, ama—ama mbegu ya hitilafu, yeze ndiye aliyekuwa na hatia ya kufanya jambo hili baya sana. Shetani alipanda mbegu yake tangu mwanzo, wakati Mungu alipoweka mavuno Yake ya kwanza ya wanadamu duniani. Adamu, bila shaka, akiwa bado anajua ya kwamba kulikuwako na ma—maarifa ya kweli, na ya mema na mabaya, naye hakuwa ameyafikia hayo bado.

13 Lakini tunaona, Mungu aliwapa watoto Wake Neno Lake liwe Ngome yao. Yao ... Hatuna Ngome nydinge ila Neno la Mungu. Hiyo ndiyo Ngome yetu. Hakuna mabomu, hakuna malazi, hakuna mahali pa kujificha, hakuna Arizona ama California, ama po pote pale; kuna ulinzi mmoja tu tulio nao, na huo ni

Neno. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu, ambaye ni Kristo Yesu, Yeye ndiye Ngome yetu pekee. Tukiwa ndani Yake, tuko salama.

Hata dhambi haihesabiwi kwa mwamini halisi. Je! Ulijua jambo hilo? Yeye aliyezaliwa na Mungu, hatendi dhambi, hawezi kutenda dhambi. Mnaona? Hata haihesabiwi. Mbona, Daudi alisema, "Heri mtu yule ambaye Mungu hatamhesabia dhambi." Unapokuwa katika Kristo, huna hamu ya kutenda dhambi. "Mwabudu, akiisha kusafishwa mara moja, hana tena dhamiri ya dhambi," hutamani. Sasa, kwa ulimwengu, huenda ukawa mwenye dhambi; bali, kwa Mungu, wewe si, kwa sababu uko katika Kristo. Unawezaje kuwa ndani ya mwenye dhambi wakati uko ndani ya yule asiye na dhambi, na Mungu anamwona Yeye tu uliyi ndani Yake?

14 Sasa wakati huu wa mavuno. Hapo mwanzo, wakati Mungu alipopanda Mbega Yake juu ya nchi na kuitoa katika mioyo ya watoto Wake, familia Yake, kulishika Neno hilo, huo ulikuwa ndio ulinzi wao pekee, kulidumisha hilo Neno! Huyu hapa adui anaingia na kuvunja kizuizi hicho, kwa kupanda mbegu ya hitilafu, kinyume cha Neno la Mungu. Kama hiyo ilikuwa ni hitilafu hapo mwanzo, bado ni hitilafu. Chochote kitakachoongeza chochote kwenye Neno la Mungu, bado ni mbegu ya hitilafu! Sijali linatoka wapi, kama linatokana na madhehebu, kama linatoka kwenye vyanzo vya kijeshi, kama linatoka kwa nguvu za kisiasa, chochote kile ambacho ni kinyume cha Neno la Mungu, ni mbegu ya hitilafu.

Wakati mtu anaposimama na kusema yeye ni mhubiri wa Injili, na kusema ya kwamba "siku za miujiza zimepita," hiyo ni mbegu ya hitilafu. Wakati mtu anaposimama na kusema ya kwamba yeye ni mhudumu, mchungaji wa kanisa la mahali fulani, naye haamini ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule kwa kila kitu (isipokuwa katika mwili wa kawaida), yeye yule jana, leo, na hata milele, hiyo ni mbegu ya hitilafu. Anaposema ya kwamba "miujiza na wakati wa mitume ulipita," hiyo ni mbegu ya hitilafu. Wanaposema, "Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu," hiyo ni mbegu ya hitilafu. Na ulimwengu umejaa hayo. Zinasongamana na kuisonga ngano.

15 Tunaona ya kwamba mpanzi wa kwanza wa mbegu ya hitilafu aliitwa "ibilisi," nasi tunajua ilikuwa hivyo, katika Mwanzo 1. Sasa tunaona, na hapa katika—katika Kitabu cha Mathayo, mlango wa 13, Yesu angali anataja hitilafu yo yote kwenye Neno Lake kuwa ni "ibilisi." Na mwaka huu wa 1956, kitu cho chote kinachopanda hitilafu, kinyume cha Neno lilioandikwa la Mungu, ama kuweka tafsiri yo yote ya kibinaksi Kwake, ni mbegu ya hitilafu. Mungu hataiheshimu. Hawezi. Haitachanganyikana. Hakika halitachanganyikana. Ni kama mbegu ya haradali; haitachanganyikana na kitu kingine chochote, huwezi kuichanganya, haina budi kuwa ndiyo kitu halisi. Mbegu ya hitilafu!

16 Sasa tunaona, wakati Mungu alipopanda Mbega Yake katika bustani ya Edeni, tunaona ya kwamba ilimzaa Hibili. Lakini wakati Shetani alipopanda mbegu yake ya hitilafu, ilimzaa Kaini. Mmoja alimzaa mwenye haki; mmoja alizaa asiye haki. Kwa sababu Hawa alilisikiliza neno la hitilafu, kinyume na Neno la Mungu, nalo lilianzisha mpira wa dhambi unaotikisika papo hapo, na umevingirishwa tangu wakati huo. Na kamwe hatutaliondoa lote mpaka malaika watakopokuja na kutenganisha kitu hicho, ndipo Mungu awapeleke watoto Wake kwenye Ufalme, na magugu yataketeketeza. Angalia hiyo mizabibu miwili.

Kama tungalikuwa na wakati zaidi juu ya somo hili, bali tu kufikia mahali pa juu sana, ili tuweze kwenda moja kwa moja kuwaombea wagonjwa katika dakika chache zijazo.

17 Angalia, mbegu zao zilikua pamoja kama tu vile Mungu alivyosema hapa pia katika mlango wa 13, wa somo letu usiku wa leo, wa Mathayo, "Zikuze pamoja." Sasa, Kaini alienda kwenye nchi ya Nodi, akajitafutia mke, na kuo; na Hibili aliuawa, na Mungu akamwinua Sethi apachukua mahali pake. Na vizazi vikaanza kusonga mbele, kati ya mema na mabaya. Sasa, tunaona walikusanyika, kila mmoja wao, wakati baada ya wakati, na Mungu ilimbidi ... Ilikuwa wovu sana hata ikambidi Mungu kuiangamiza.

Lakini hatimaye walitokea mpaka mbegu hizo mbili, mbegu ya hitilafu na Mbega ya Mungu, zikatokeza vichwa vyao halisi, na jambo hilo likakamilishwa katika Yuda Iskariote na katika Yesu Kristo. Kwa kuwa, Yeye alikuwa ni Uzao wa Mungu, Yeye alikuwa mwanzo wa kuumba kwa Mungu, Yeye hakuwa kitu ila Mungu. Na Yuda Iskariote alizaliwa mwana wa upotevu, alitoka kuzimu, akarudi kuzimuni. Yesu Kristo alikuwa ni Mwana wa Mungu, Neno la Mungu lililodhihirishwa. Yuda Iskariote, katika hitilafu yake, alikuwa ni uzao wa Ibilisi, aliyejuwa ulimwenguni, na kwa ajili ya udanganyifu; kama tu alivyokuwa hapo mwanzo, Kaini, baba yake wa zamani.

18 Yuda alicheza tu kanisani. Yeye hakuwa mwaminifu kabisa. Kwa kweli hakuwa na imani; asingemsaliti Yesu kamwe. Lakini, mnaona, yeye alipanda hiyo mbegu ya hitilafu. Alifikiri ya kwamba angeweza kufanya urafiki na ulimwengu, mali, na pia kuwa na urafiki na Yesu, lakini alikuwa amechelewa sana kufanya jambo lo lote kuhusu jambo hilo. Wakati ile saa ya kuwa ilipowadia, wakati alipofanya jambo hili ovu, alivuka mstari wa kutenganisha kati ya kwenda mbele na kurudi. Ilimbidi kuendelea katika njia aliyoinedea, kama mdanganyifu. Yeye alipanda mbegu ya hitilafu, alijaribu kupata kibali kwa hayo madhehebu makubwa ya siku hiyo, na Mafarisayo na Masadukayo. Naye alidhani angejitetengeneza kipande cha fedha, na angependwa na watu. Kama hilo halisababisha watu wengi sana kuingia katika hitilafu hiyo, wakijaribu kupata kibali kwa wanadamu! Hebu na tupate kibali kwa Mungu, si kwa mwanadamu. Lakini hivyo ndivyo

Yuda alivyofanya wakati hitilafu hizi zilipoingia ndani yake.

19 Nasi tunajua ya kwamba Yesu alikuwa Neno, Yohana Mtakatifu 1, ilisema, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa hapa mionganoni mwetu." Halafu, Neno ni Mbega, kisha Mbega ikawa mwili ikakaa kwetu.

Kama Yuda alikuwa ni uzao wa adui na hitilafu, pia ulifanyika mwili na kukaa mionganoni mwetu katika nafsi ya Yuda Iskariote. Yeye kamwe hakuwa na imani halisi, halisi. Alikuwa na kile alichodhani ni imani. Kuna kitu kama kuwa na imani; na imani ya kujifanya.

Na imani halisi ya Mungu itamwamini Mungu, na Mungu ni Neno, kamwe haitaongeza kitu Kwake. Biblia inatuambia kama tukiongeza neno moja, ama kuondoa Neno moja, sehemu yetu itaondolewa kwenye Kitabu cha Uzima, Ufunuo 22:18, mlango wa mwisho wa kumalizia.

20 Katika mwanzo wa kwanza, Kitabu cha kwanza cha Biblia, Mungu aliwaambia wasivunje Neno moja la Hilo, "kila Neno halina budi kutunzwa," hawana budi kuishi kwa Neno hilo. Yesu, katikati ya Kitabu, alikuja na kusema jambo hilo katika Wakati Wake, na kusema, "Mtu hataishi kwa mkate tu, bali kwa kila Neno ambalo—litokalo katika kinywa cha Mungu." Na katika wakati wa kumalizia wa Ufunuo, uliotabiriwa kwetu, ya kwamba "Mtu ye yote atakayeondoa Neno moja katika Kitabu, ama kuongeza neno moja Kwake, sehemu yake itaondolewa kwenye Kitabu cha Uzima."

Kwa hiyo hapawezi kuweko na kitu cho chote kisicho cha hakika, ni Neno tu halisi la Mungu, lisiloghoshiwa! Hao ni wana wa Mungu, binti za Mungu, wasiozaliwa kwa mapenzi ya mwanadamu, wala kwa kupeana mkono, wala aina fulani ya ubatizo; bali wamezaliwa katika Roho wa Mungu, kwa Roho Mtakatifu, na Neno likijidhihirisha lenyewe kupitia kwao. Hiyo ni Mbega halisi ya Mungu!

21 Adui hujiunga na kanisa na anakuwa wa kweli sana katika kanuni ya imani ama kitu fulani. Lakini hiyo si ... Hiyo ni hitilafu, kitu chochote kinachoingilia aina hiyo ya Ukweli halisi wa Neno la Mungu.

Na tunajuaje? Tunasema, "Vema, wao, una haki ya kulifasiri?" La, bwana! Hakuna mtu aliye na haki ya kufasiri Neno la Mungu. Yeye ni mfasiri Wake Mwenyewe. Yeye huliahidi, kisha analitimiza, hiyo ndiyo tafsiri yake. Wakati alipoliahidi, basi Yeye analitimiza, hiyo ndiyo tafsiri Yake. Chochote kinyume cha Neno la Mungu ni hitilafu! Kabisa!

Sasa, kama nilivyosema, Yuda hakuwa na imani halisi. Alikuwa na imani ya kujifanya. Alikuwa na—na imani ambayo alifikiri ya kwamba huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu, bali hakuja huyo alikuwa ni Mwana wa Mungu. Asingefanya hivyo. Na mtu ambaye atapatana juu ya Neno hili la Mungu kuwa ni Kweli, yeye ana imani ya kujifanya. Mtumishi halisi wa Mungu atashikilia Neno hilo.

22 Siku chache zilizopita usiku, mhudumu fulani, wa Arizona, wa shule kuu na maarufu hapa katika mji huu, alinjia na kusema, "Na—nataka kukunyoosha juu ya jambo fulani" (nikasema ...) "utakapopata nafasi."

Nikasema, "Hii ndiyo nafasi nzuri sana niijuayo. Njoo huku."

Na kwa hiyo akaja, akasema, "Bw. Branham, unajaribu ... Ninaamini wewe ni mwaminifu na wewe ni mwaminifu, bali unajaribu kuingiza ulimwenguni Fundisho la kimitume." Na akasema, "Wakati wa mitume ulikoma pamoja na mitume."

Nikasema, "Jambo la kwanza ningetaka kukuuliza, ndugu yangu, unaamini ya kwamba kila Neno la Mungu limevuviwa?"

Akasema, "Naam, bwana, hakika ninaamini."

Nikasema, "Basi, ungeweza kunionyesha katika Neno ambapo wakati wa mitume ulikoma? Sasa, nionyeshe ilipo, nitaamini pamoja nawe." Nami nikasema, "Mwandishi wa mitume, yule aliye kuwa na funguo za Ufalme, kwenye siku ya Pentekoste wakati ule wakati wa mitume ulipoanzishwa, wao walismesa, 'Enyi watu na ndugu, tufanye nini tupate kuokolewa?' Yeye alisema, 'Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu, kwa kuwa ahadi hiyo ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, na kwa hao walio mbali, na wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu. Sasa, Neno linawezaje kujipinga?"

Yule mtu akasema, "Nina baridi kali sana usiku wa leo."

Nikasema, "Nafikiri hivyo, pia." Mnaona?

Sasa wewe niambie, je! Mungu angali anaita? Kama Mungu angali anaita, basi wakati wa mitume ungalipo. Hakika! Bila shaka! Wengi watakaoitwa na Bwana Mungu wetu, watakapata kuitwa, watakaoitwa wakati wo wote, wote atakaowaita Yeye, ungalii utakuwa ni wakati wa mitume, kwa kuwa Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

23 Sasa, tunaona leo ya kwamba hitilafu hii imepandwa katika kila wakati. Kama ingaliwezekana kulipata katika dakika kumi ama kumi na tano zijazo, ningefanya hivyo, bali huwezi. Kote katika nyakati ... Sisi sote, karibu sote tunasoma Biblia. Na sasa kama vile Yesu alipokuja, Naye akakuta hiyo hitilafu, kinyume. Yeye alikuwa Neno liliodhihirishwa, Yeye alikuwa ni tafsiri ya Mungu ya Neno, kwa sababu Yeye alisema, "Yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa ndani Yake mnafikiri mna Uzima wa Milele, na hayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi." Haya basi. Yeye—Yeye alikuwa ndiye tafsiri ya Neno. Na kila mwana na binti wa Mungu aliyezaliwa mara ya pili ni ufasiri wa Neno. Ninyi ni nyaraka zilizoandikwa, zinazosomwa na watu wote. Ndiyo.

Angalia, Yeye alisema, "Wananiabudu bure, wakifundisha hitilafu kwa Mafundisho. Wananiabudu bure, wakifundisha Mafundisho hitilafu, mafundisho ya mwanadamu, kanuni za imani za mwanadamu, wakifundisha hilo kuwa ni Neno la Mungu, wakati halina uhusiano wo wote na Neno la Mungu."

24 Angalia, kila wakati unazaa mazao kama hayo, kila wakati umefanya hivyo, na yetu si udhuru. Tuna jambo lile lile, na wakati wake mkuu kuliko nyakati zingine zote zilizowekwa pamoja, kwa maana huu ndio mwisho wa historia ya ulimwengu. Hii ndiyo hitilafu kuu iliyowahi kuwa juu ya nchi, iliyu juu ya uso wa dunia leo. Hitilafu katika nyakati zingine iliwaondoa kwenye Mungu wa kweli na aliye hai, wakaenda kwa sanamu. Leo, Yesu alisema katika Mathayo 24:24 ya kwamba ingekuwa karibu sana, ingewapoteza walio Wateule kama yamkini. Nena kuhusu hitilafu! Loo, ni janja sana. Shetani yuko mionganoni mwa watu, na mwanatheolojia kama huyo, Daktari wa Uungu, anaweza kufundisha Neno hilo karibu kabisa. Yesu alisema hivyo. Lakini mwangalie tu, kutakuwa na mahali fulani. Kasema, "Vema, sasa, hiyo haikuwa kwa ajili ya jambo hili." Loo, naam, ndivyo ilivyo, pia, unaona, kwa sababu Mungu alisema ilikuwa hivyo.

25 Angalia kile illichofanya. Hitilafu ile ile ililetä hasira ya Mungu juu ya siku za Nuhu, wakati Mungu alipomtuma nabii Wake nje na kuhubiri kama moto uwakao, uliwaita watu kutubu, na hitilafu ikazama. Basi Shetani alifanya nini? Akaja moja kwa moja nyuma, katika Hamu, na akaanza kuipanda tena. Hiyo ni kweli kabisa.

Kisha akaja Musa, yule nabii mkuu, kuwatoa wana wa Israeli kutoka jangwani. Ni kitu gani kilichotukia? Musa, nabii mkuu wa Mungu, akiwaletea Kweli kabisa, Kweli iliyothibitishwa. Alikuwa amekutana na Mungu. Mungu alithibitisha ya kwamba alikuwa amekutana Naye. Jinsi ambavyo watu hao kule nyuma, hao makuhani, nao walikuwa na dini zao, taratibu zao, ibada zao na kila kitu, bali Musa alisimama kama thibitisho la tafsiri ya Neno. Usisahau jambo hilo! Musa alikuwa ndiye fasiri ya Mungu ya ahadi Yake. Yeye alisema angefanya hivyo; alikuwa ndiye fasiri ya Mungu.

26 Ni kitu gani kilichotukia? Kanisa lilianza tu kutoka Misri, kwa miguu yake siku chache, na ni kitu gani kilichotukia? Shetani alikuja pamoja na hitilafu yake katika mtu, Kaini wa pili, ambaye alikuwa Balaamu, naye akapanda hitilafu mionganoni mwao. Tunajua hiyo ni kweli. Ya kwamba Balaamu, mafundisho ya Balaamu, ya kwamba "sisi sote ni ni kitu kimoja, tunamtumikia Mungu yeye yule mnayemtumikia," kimsingi, yeye alikuwa sahihi, kwa maana alitoa sadaka ambayo Mungu alitoa; kondoo dume saba, fahali saba kwenye madhabahu saba, na kuomba kwa Mungu yeye yule kikamilifu kabisa kama vile Musa alivyofanya kule jangwani, namna ile ile kabisa. Lakini hawakuwa sawa! Ikituvekea kivuli cha yale yatakayotukia. Kulikuwako, tena, Kaini akidhihirishwa katika u—utu wa Balaamu. Na kulikuwa na Mungu akidhihirishwa katika utu wa Musa, akifasiri Maneno Yake kuititia kwa mwanadamu, akijitambulisha Mwenyewe, ahadi Yake, kuititia kwa mwanadamu. Ndipo hitilafu ikainuka.

Vivyo hivyo ilifanya hivyo katika wakati wa Yuda, huyo hapo akaja na hitilafu yake.

27 Na, kumbukeni, dhambi hii ambayo watu hao waliamini, ya kwamba "sisi sote ni sawa, tunamwabudu Mungu yule yule, sote tunapaswa kuwa wa kanisa moja, tunapaswa kuwa watu wale wale," dhambi hiyo haikusamehewa Israeli kamwe! Yesu alisema, Mwenyewe, "Wote wamekufa!"

Waliangamia, wote isipokuwa watatu. Hao ndio walioshikilia na kuamini ile ahadi. Wakati waoga waliposema, "Hatuwezi kuitwaa hiyo nchi, na ni kazi kubwa sana kwetu," na kadhalika; Kalebu na Joshua wakawatuliza watu, na kusema, "Sisi tunaweza hata na zaidi kuiteka, kwa maana Mungu alituahidia hiyo! Sijali upinzani ni nini!"

Nasi bado tunaweza kuhubiri uponyaji wa Kiungu, na ubatizo wa Roho Mtakatifu, na bado tuna nguvu za Mungu kututenganisha na mambo ya ulimwengu. Mungu alisema hivyo! Wakati wa mitume haujakoma kamwe, wala hautakoma, unaendelea.

Kwa hiyo, tunamwona mpanzi yule yule wa kale wa hitilafu. Na kumbuka, dhambi hiyo haikusamehewa kamwe. Sasa, ndugu, kama haikusamehewa wakati huo, viyi sasa wakati ile—ile mbegu halisi ya nyakati zote inapokusanyika pamoja?

28 Angalia jambo hili kuu ambalo Balaamu alifanya, liliendelea na kuendelea, na hatimaye likaishia katika kuja kwa—kwa Yuda Iskariote, na Yesu. Ilikuwa ni kitu gani? Yuda na Yesu walikuwa mfano halisi wa Kaini na Habili. Kwa kuwa, kama vile Yuda alivyokuwa wa kidini, vivyo hivyo na Kaini alikuwa wa kidini. Kaini

alijenga madhababu, alitoa dhabihu, alimwabudu Mungu, alikuwa mwaminifu tu ndani yake kama yule mwininge alivyokuwa. Lakini, unaona, yeye hakuwa na ufunuo wa kile Neno lilikuwa. Alidhani ilikuwa ni Adamu na Hawa waliokula matofaa ama tunda fulani. Na Kaini ... Habilii, kwa ufunuo, alijua ya kwamba ilikuwa ni makosa; damu ndiyo iliyowatoa, naye akamtoa mwana-kondoo. Naye Mungu akashuhudia sadaka yake ilikuwa ni kweli. Ndipo akawa na vivu na kujaribu kumwua ndugu yake. Na wakati alipomwua ndugu yake juu ya madhababu ile ile ambayo dhabihu yake ilifia, mwana-kondoo alikuwa juu ya madhababu, vivyo hivyo Yuda Iskariote alimsaliti Yesu Kristo juu ya madhababu ya Mungu, na kumwua kama tu Kaini alivyomwua Habilii. Kwa sababu, Kaini alikuwa mzao wa hitilafu.

Na vivyo hivyo na Balaamu, nabii wa kukodiwa, mtu ambaye alipaswa kujua vizuri zaidi. Na Mungu alimwonya kwa ishara na maajabu, na hata nyumbu akinena kwa lugha zisizo julikana, na hata hivyo aliendelea tu vivyo hivyo. Yeye alizaliwa awe m—mpanzi wa hitilafu.

29 Na kama Yesu alitabiri wakati huu utaishia kwenye hitilafu kuu sana iliyowahi kuwa, wakati wa kanisa la Laodikia, vuguvugu, ambao ulimtoa nje ya kanisa, ingewezaje kuwa kitu kingine cho chote ila ile hitilafu! Hakika, ndivyo ilivyo. Inaishia katika wakati huo.

Na ilikuwa ni Kaini na Habilii tena pale Kalvari.

Sasa angalia, kama ilivyokuwa, mara tu Yesu alipoondoka, akaenda Mbinguni, Roho Mtakatifu alirudishwa. Huyo alikuwa ndiye yule Mzao, mto-Uhai kwa Neno, kama tulivyonena jana usiku. Huyo ndiye Mwenye kulihuisha Neno. *Kuluisha* maana yake ni "kufanya Hai." Roho Mtakatifu halisi hulifufua Neno tu ilivyo. Haitaleta kanuni ya imani kwenye Uzima, haiwezi, kwa sababu si kitu cha kanuni ya imani. Ni Uzima wa Neno la Mungu, kwa kuwa ni Mungu. Mnaona? Naye huuhiusha huo Mwili.

30 Sasa angalia, kama walivyofanya. Sasa angalia, kama walivyofanya. Halafu, kama vile Biblia ilivyo sema, na—na Yohana alinena na watoto wake, na kusema, "Watoto wadogo, mmesikia habari za mpinga-Kristo aliye kuwa aje ulimwenguni," kasema, "ambaye tayari yuko ulimwenguni, na anafanya kazi katika wana wa kuasi." Sasa, hiyo ilikuwa karibu miaka thelathini baada ya kuja kwa Roho Mtakatifu. Tunaona, wakati Roho Mtakatifu alipokuja, yule Mzao halisi, Mpaji halisi wa Uhai kwa ile Mbegu, basi hapa inakuja hitilafu hiyo tena. Na tazama, hilo likaendelea. Ilikuwa ...

Lile Neno halisi lilikuwa limethibitishwa, hao manabii wa kale walikuwa wamelithibitisha Neno la Mungu kuwa ni Kweli walipokuwa wanaaga dunia. Kama mtu ye yote alipata kusoma lile gombo la Baraza la Nikea, ama la Baraza Lililotangulia Nikea, hizo siku kumi na tano za siasa za umwagikaji wa damu, wakati hilo kundi la Warumi kule chini lilipotaka kuingiza na kuunda madhehebu kutokana na kanisa hilo. Manabii waliingia, wamevikwa ngozi ya kondoo, wakila mboga, na kulitetea Neno hilo! Lakini ilifanya nini? Ilibidi iwe kama Kaini, ilibidi iwe kama Habilii, mmoja ilibidi afe. Hakika, ilikuwa hivyo. Na Neno likapoteza ushawishi Wake kati ya watu, nao wote wakalikataa Neno la kweli na kuchukua mafundisho ya sharti ya hitilafu za kanisa Katoliki la mwanzoni. Wakaongeza papa, wakaongeza askofu, wakaongeza *huyu, yule*, yule *mwininge*. Waliondoa maana halisi ya Petro, na ya—ya—ya Mariamu, na—na mengine yote; na kufanya sanamu, na hawakufanya kitu ila ibada tu ya kipagani kutokana na kile kinachoitwa dini ya Kikristo. Ilikuwa ni kitu gani? Mbegu ya hitilafu! Na wakaunda madhehebu, wakaunda madhehebu, kwa mara ya kwanza duniani, kanisa. Ilikuwa ni kitu gani? Hiyo mbegu ya hitilafu ambayo ilianza kupandwa, kitu fulani kikiongezwa, kikiondolewa.

31 Ni nani aliywahii kusikia, katika Biblia, kutokula nyama Ijumaa? Ni nani aliywahii kusikia, katika Biblia, juu ya kitu chochote cha kunyunyizia badala ya kubatiza, kuzamisha? Ni nani aliye pata kusikia mambo hayo, "Salamu, Mariamu" ama kitu kama hicho? Ni nani aliywahii kusikia baadhi ya haya maovu yaliyooza ya Waprotestanti hawa, pia? Chungu hakiwezi kusema birika ina grisi. Sawa! Ni ninii tu, mwenye hatia ya jambo dogo ana hatia ya yote! Ni nani aliywahii kusikia Mungu akifanya kazi katika madhehebu? Nioneshe wakati wo wote ambapo mmoja alipata kuunda madhehebu na akaendelea kuwa hai. Walikufa mara moja, wala hawakufufuka tena! Ni wakati ambapo jambo fulani linatukia, ni wakati wa Mungu kusogea. Iliua ushawishi mionganii mwa watu.

Jambo lile lile limefanywa leo. Wanaua ushawishi, wanasema, "Loo, kundi hilo la watakatifu wanaojifingirisha, hawana kitu." Na, mbona, ni hitilafu! Kutana na Neno uso kwa uso na uone ni kitu gani, uone kama Mungu hufasiri Neno Lake Mwenyewe. Mungu anaweza kutoka kwa mawe haya kumwinulia Ibrahimu watoto. Amina.

32 Neno lilikuwa limethibitishwa kweli kweli na hao Wakristo wa mwanzoni, jinsi Mungu alivyowaokoa kutokana na kila kitu, na magonjwa, nao walikuwa na manabii, nao walineni kwa lugha, wakafasiri, na wakatoa jumbe ambazo zilitokea kuwa ni kweli kabisa kila wakati. Lakini licha ya Neno hilo lote ililothibitishwa, watu walilikataa Hilo, na kuchagua madhehebu. Huyo ni mama wa madhehebu yote.

Zote mbili zimekomaa kabisa sasa. Zilianza kutoa mbegu tena. Ilikuwa, bali ikachanua tena katika siku za Luther, kama tunavyo jua kutoka kwenye jumbe zilizotangulia hapa katika ile asubuhi ya kiamshakinywa. Ilichanua katika siku za Luther. Sasa walifanya nini? Mara baada ya mtu huyo mkuu kufa,

wakaunda madhehebu.

Ilichanua. Na tena katika siku za John Wesley, wakati hao Waanglikana, hata pamoja na usalama wao wote wa milele na kila kitu kilikuwa kimeufunga kufikia mahali ambapo ilikuwa karibu ni ya kuenea mahli pote, basi ni jambo gani lilitukia? Mungu alimwinua mtu jina lake John Wesley, na kuua kitu hicho chote. Na mara alipokuwa, yeye na Asbury na hao wengine, ni kitu gani kilichotukia? Waliunda madhehebu, na sasa mna kila namna ya Wamethodisti. Ndipo akaja mmoja au mwingine, Alexander Campbell, John Smith, na kadhalika.

33 Hatimaye, Pentekoste ikavunjika, ikitoka kwa yote hayo. Ilikuwaje basi? Walikimbia vizuri, ni kitu gani kiliwazuia? Mlirudi moja kwa moja kwenye matope yale yale mliyotoka, mkarudi kwenye matope yale yale, mkarudi kwenye hitilafu na kufanya madhehebu, iliwabidi kupatana juu ya Neno. Na kila wakati Mungu angetuma kitu kipyta, usingeweza kukipokea. Hiyo ni kweli! Hitilafu tena! Na, angalieni, kama nilivyo sema hivi majuzi, ya kwamba hilo ganda la kwanza dogo lililotoka kwenye shina hili, linatoka likawa majani kisha linakuwa shada, kisha linearudi likawa ubua tena, halafu linatoka. Lile ganda dogo la ngano karibu linafanana na punje yenewe, nasi tulifikiri ilikuwa hivyo, bali unapoifungua, hamna punje kule hata kidogo. Ni msaidizi tu wa punje kukua, na pia hufa, na uhai unatoka ndani yake na kuingia kwenye punje. Angalia, kwa hiyo wanaita makanisa yaliyopanda ...

34 Tunaona siku hizi ya kwamba yale tunayoita makanisa, hata kwa Wapentekoste wetu, tulitoka, hatukuweza kuridhika, ilitubidi kufanya makundi yetu wenewe. Kila kitu kilitokea, ilitubidi kuwa na *hili*, ilitubidi kuwa na *hili*, ilitubidi kuunda kundi lingine. Na jamaa huyu akainuka, kasema, "Yeye yuaja juu ya wingu jeupe." Mwingine anasema, "A-ha, Yeye anakuja juu ya farasi mweupe." "Vema, tutafanya makundi mawili." Mnaona, ni kitu gani? Kupanda hitilafu! Atakapokuja, cho chote kile, Yeye atalifasiri Neno Lake Mwenyewe atakapokuja. Hebu na tongoje mpaka wakati huo. Chukua ninii ... Ukizungumza juu ya jambo hilo, hata huupati Ujumbe wa siku hii. Daima akionyesha kile Mungu atakachofanya, ama kile Yeye amefanya, na kupuza kile anachofanya. Hivyo ndivyo tunavyopata hitilafu ndani yake.

35 Sasa tunaona ya kwamba leo makanisa yetu, makanisa yetu yote—yote yamepanda upepo, na yanavuna tufani. Hatuna mikutano ya maombi, hatuna ibada tulizo kuwa nazo. Kuna nini? Tumeachilia kila kitu. Angalieni, hata kwa makanisa yetu ya Kipentekoste, yameketi yamejaa wanawake waliokata nywele zao. Hilo lilikuwa haliruhuswi. Nyuso zilizopodolewa, wamepaka rangi kwenye kucha, kila namna ya upuuzi; wanampata mtu hapa nje mwenye...Kama akina Rickey na kadhalika; wameoa mara tatu ama nne, na ni mashemasi; loo, ni hitilafu ya jinsi gani! Ni uchafu! Wanafanyaje jambo hilo? Mungu hataruhusu jambo hilo Kanisani Mwake, inawabidi kwenda kwenye madhehebu wapate kufanya jambo hilo. Mtu fulani anaogopa kusema jambo fulani juu yake, maana wangefukuzwa kwenye madhehebu. Mungu, tupe watu ambao hawajaunganishwa na cho chote ila Mungu na Neno Lake, ambao watasema Ukweli juu ya jambo hilo. Hilo ndilo hasa tunalohitaji. Tumefanya nini? Tumepanda hitilafu. Tumepanda upepo, na sasa tunavuna upepo tufani.

36 Angalia ya kwamba sasa wanakusanya pamoja kwa ajili ya kuchomwa moto. Je! Umeng'amua, Yesu alisema, "Kwanza, yakusanye pamoja, yafunge matita matita, kisha uweke matita hayo kwenye lundo moja, Nami nitayateketeza." Kuna kifungu kidogo kinachoitwa Methodisti, Baptisti, Presbiteri, Lutheran, wote wanakusanya pamoja katika Baraza la Makanisa Ulimwenguni. Ni kitu gani? "Wakusanye kwanza!" Haleluya! Je! Ulipata kuona, Yeye kwanza anakusanya magugu, anayaondoa kwenye ngano, anayatenganisha, "Yakusanyeni pamoja na mkayateketeze." Yote yatakeketeza kwa hukumu za Mungu, kwa sababu ya kupanda hitilafu kati ya watu, mambo ambayo wao... Wakiwa na mfano wa utauwa, na wakikana Nguvu zake, wakikana Neno, kushikilia tu ibada fulani za kidini, za mafundisho ya sharti ambayo mtu fulani ameingiza ndani, akijaribu kuweka katika Neno la Mungu. Haitafaa kitu. Ni hitilafu.

37 Ninapaza sauti leo, kama ilivyokuwa, nabii mkuu wa zamani za kale, Amosi, wakati aliposhuka kuja kwenye mji huo, alisema, "Mimi si nabii, wala mwana wa nabii. Lakini kama simba akinguruma, ni nani asiyeweza kuogopa!" Yeye alisema, "Mungu anapozungumza, ni nani asiyeweza kutoa unabii." Yeye alitabiri hukumu juu ya kizazi hicho, kasema, "Mungu yule yule mnayedai kumtumikia atawaangamiza."

Wekeni jambo hili, liko kwenye kanda, na mkumbuke. Mungu yule yule ... Watu hawa sasa wanaokusanya mavuno haya yote makubwa ya—ya Baraza la Makanisa Ulimwenguni, nanyi itawalazimu kuingia humo. Huwezi kukaa nje yake. Aidha mtaondoka humo mtu mmoja mmoja, la sivyo mtaingia humo. Hakutakuwako na msimamo wa katikati. Itakuwa ni alama ya mnyama. Hakuna mtu angaliweza kununua wala kuuza, isipokuwa yeye aliye na alama, ama aliye na hitilafu. Sasa, tokeni kwake! Tokeni kwake! Ikimbieni! Kaeni mbali nayo! Mungu ambaye wanadai wanamtumikia atawaangamiza. Mungu mkuu wa upendo ambaye hataninii ...

Kasema, "Vema, Yesu aliomba ya kwamba sisi sote tunapaswa kuwa mmoja."

38 Ndipo Yeye pia akasema, "Mnawezaje kutembea pamoja, wawili watembe pamoja, wasipopatana?" Yeye alisema "mmoja," kama vile Yeye na Baba walivyo Mmoja. Naye Baba alikuwa ni Neno, Naye alikuwa Neno lililodhihirishwa. Yeye alikuwa "Mmoja" pamoja na Baba, kwa sababu Yeye alikuwa dhihirisho la Neno

Ia Mungu lililoahidiwa. Na ndivyo ilivyo leo, ama siku nyingine yoyote. Naam, bwana. Mungu ni Mmoja. Yeye anatutaka tuwe mmoja.

Inawezekanaje *hawa wawe ni mmoja, huyu akikana kuzaliwa kibikira, na huyu haamini, anakana kuponya Kiungu, na huyu, yule, hao wote wakiwa katika mchafuko jinsi hiyo?* Wengine wao hata hawamwamini Mungu, wanaamini alikuwa Mwana wa Mungu; wanaamini Yeye alikuwa ni mwana wa Yusufu, *aliyeitwa* Mwana wa Mungu. Hakika. Yule ndugu mapacha kwa Walutheri, Wazwingli, wanaamini jambo hilo, ya kwamba Yeye alikuwa ni mtu mzuri tu. The Christian Science ilisema Yeye alikuwa ni nabii, mtu wa kawaida tu, Yeye hakuwa wa Kiungu. Mbona, kama Yeye hakuwa wa Kiungu, Yeye ndiye mdanganyifu mkuu sana ulimwengu uliyewahi kuwa naye. Yeye alikuwa Mungu ama hakuwa kitu. Yeye alikuwa wa Kiungu! Yeye alikuwa Mungu, Mwenyewe, aliyefanyika mwili mionganoni mwetu, katika utu wa Mwana wa Mungu. Hakika, hivyo ndivyo alivyokuwa.

39 Sasa tunaona hitilafu imeingia. Tunajua ya kwamba liko hapa, hakuna mtu anayeweza kukana jambo hilo. Loo, jamani! Angalia tu. Yeye ataliangamiza kundi hilo linalodai linamtumikia Mungu. Wewe angalia.

Mungu alipanda Mbegu Yake. Ninafunga, maana ni wakati wa kuanza mstari wa maombi. Mungu alipanda Mbegu Yake, na Mbegu Yake ni Kristo. Nitahubiri juu ya jambo hilo katika siku chache usiku, mahali ambapo Mungu aliamua kuweka Jina Lake, Bwana akipenda, labda kwenye moja ya viamshakinywa wakati nikiwa na wakati kidogo wa ziada. Angalia, Yeye Ndiye Njia pekee ya kuepukia. Ndiye Mtawala pekee wa kweli. Yeye ndiye Mungu pekee wa kweli, hakuna mwingine ila Yeye. "Mimi ni Mungu, na Mungu peke Yangu," Yeye alisema. Yesu alisema, "Hii ndiyo amri: Sikilizeni, enyi Israeli, Mimi ni Bwana Mungu wenu, Mungu mmoja tu. Mimi Ndimi. Kwa nini unatafuta mwingine? Mwingine atakuja ... Ninakuja katika Jina la Baba Yangu, nanyi hamnipokei. Lakini mwingine atakuja kwa jina lake mwenyewe, naye mtampokea." Nao walifanya hivyo huko Nikea.

"Je! Wewe ni Mkristo?"

"Mimi ni Mbatisti."

"Je! Wewe ni Mkristo?"

"Mimi ni Pentekoste."

"Je! Wewe ni Mkristo?"

"Mimi ni Mmethodisti," jina lingine.

40 Bali inapofikia kwenye Jina hilo la "Yesu Kristo," wanaenda mbali na Hilo wavezavyo, hawataki uhusiano wo wote Nalo, kwa kuwa Yeye ni Neno na Neno hujitangaza Lenyewe. Angalia, Njia pekee ya kuepukia! Yeye ni Ua la Uwandani, Biblia ilisema alikuwa. Kila cheo (katika Biblia) cha Mungu ni cha Yesu Kristo. Yeye alikuwa Alfa, Omega, Mwanzo na Mwisho; Yeye aliyeuwako, aliye, na atakayekuwa; Shina na Mzao wa Daudi, Shina na Mzao wa Daudi; Nyota ya Asubuhi, Ua la Uwandani, Nyinyoro ya Mabondeni, Alfa, Omega, Baba, Mwana, Roho Mtakatifu, yote katika Yesu Kristo! Yeye alikuwa dhihirisho kamili la Yehova Mungu aliyefanyika mwili kukaa kati yetu. Kile hasa alichokuwa.

Yeye alikuwa ni Ua la Uwandani. Walifanya nini na Ua la Uwandani? Walilikamua, wakaliponda, wapate kutoa manukato Kwake. Ua nzuri la waridi halina budi kukamuliwa sana ili kupata manukato kutoka kwenye hilo ua la waridi. Na hayo yalikuwa ni Maisha yanayopendeza, hakujapata kuwako na maisha yaliyoishiwa kama Yeye, lakini ilibidi akamuliwe huko Kalvari.

41 Unaona, wao walichukua u—upako wa Ua la Uwandani na kuuweka juu ya Haruni, ilibidi atiwe mafuta hayo apate kuingia mbele za Bwana katika mahali patakatifu, katika pazia takatifu. Ilimpasa atiwe mafuta ya Ua la Uwandani, apate kuingia kukinyunyizia kiti cha rehema kila mwaka. Na upako huo hauna budi kuwa juu yake, harufu nzuri mbele za Bwana, akibeba damu ya mwana-kondoo mbele yake, baada ya yeye pia kunyunyiziwa na mwana-kondoo. Komamanga na kengele zikiwa zimezunguka mavazi yake, naye ilibidi atembee kwa hatua fulani, zikiimba "mtakatifu, mtakatifu, mtakatifu kwa Bwana."

42 Angalia, Yeye ni lile Ua la Uwandani, ile Harufu tamu na nzuri, ule Upako juu ya watu Wake. Huwezi kuja mbele Zake ukiwa na kanuni yoyote ya imani, kitu kingine chochote, bali umepakwa mafuta ya hilo Ua la Uwandani, lile Neno. Yeye pia ni Yungiyungi la Bondeni.

Sasa, unapataje bangi? Unapata bangi wakati unapochukua yungiyungi na kulikamua, unapata bangi. Madaktari wanaitumia katika maabara zao. Mchukue mwanaume aliye na wasiwasi na mwenye mahangaiko, ama mwanamke, anayejisikia kama kwamba ataingia kichaa, anayetembea sakafuni na kupiga mayowe, mwenye wazimu, daktari atachukua bangi yake kidogo ya yungiyungi na kuiingiza ndani ya mkono wake ama ya vena mahali fulani, ama mwanamume, nao watatulia. Yote yamekwisha kwa muda kidogo. Lakini mara tu hiyo bangi inapoisha, hawa hapa wanakuja tena, ni wabaya kuliko walivywahi kuwa.

43 Ila nitawaambia, enyi marafiki, hiyo ni mfano tu wa ile Bangi halisi kutoka katika Ua la Mabondeni ninalojuua. Yeye ni Ua la Mabondeni. Alikamuliwa pale Kalvari. Alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa kupigwa Kwake sisi tumeponywa. Katika hilo, kule kukamua kutoka kwenye maua, Yeye alikuwa ni Ua. Alikuwa Ua kuu sana kuliko yote lililopata kuota, ilikuwa ni hili Ua la Mabondeni, na hili Waridi kuu la Uwandani. Sasa Yeye ananing'inia usiku wa leo, ameangikwa kati ya Mbingu na nchi, ninaamini, alikuwa hivyo wakati huo, hasa, a—apate kuondoa dhambi ya ulimwengu na kurudisha uponyaji kwa ulimwengu. Na Biblia ilisema ya kwamba ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

44 Ewe rafiki, wakati Mungu alipomwambia Musa, kule jangwani, ambaye alikuwa ni m—mfano Wake, alimwinue nyoka wa shaba. Na shaba inawakilisha dhambi iliyohukumiwa, nyoka anawakilisha, *nyoka wa shaba* anawakilisha "dhambi iliyohukumiwa tayari." Kama vile, *shaba* ni "hukumu ya Kiungu," kama madhabahu ya shaba ambapo dhabihu ziliwekwa. Na pia Eliya aliangalia juu na kusema ya kwamba mbingu zilikuwa kama shaba, hukumu ya Kiungu juu ya taifa lisiloamini ambalo lilikuwa limerudi nyuma kutoka kwa Mungu. Shaba inawakilisha hukumu, hukumu ya Kiungu. Naye nyoka aliwakilisha dhambi iliyohukumiwa tayari; na Yesu ndiye yule nyoka aliyefanywa dhambi kwa ajili yetu, na akachukua hukumu za Mungu juu Yake. Alijeruhiwa kwa makosa yetu, akachubuliwa kwa maovu yetu, adhabu ya amani yetu ilikuwa juu Yake, na kwa kupigwa Kwake sisi tumeponywa.

Loo, Mungu ana kabati lililojaa Bangi, usiku wa leo, kwa ajili yako. Rafiki Mkristo, wewe ni mgonjwa na unateseka. Loo, umechoka, ni vigumu sana kwako. Huwezi kustahimili kwa muda mrefu zaidi, uta—utaingia kichaa katika siku hizi za kisasa tunazoishi.

45 Je! Mlisikia tu *Life Line* usiku wa leo, ya kwamba yale waliyosema, ambayo—ambayo Urusi inasema, mnamo mwaka wa '55, ya kwamba "watautawala kabisa ulimwengu mzima"? Kabla jambo hilo halijatukia, kunyakuliwa hakuna budi kuja. Kwa hiyo ni karibu vipi, rafiki? Iko papa hapa karibu sasa.

Hivi hutamtafuta usiku wa leo kwa moyo wako wote? Yeye ni Nyinyoro ya Mabondeni, na ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Yeye yuko hapa usiku wa leo kujiinua Mwenyewe mionganoni mwa watu Wake, kama tu vile Musa alivyoinua ile—ile ishara ya dhambi, aliyohukumiwa. Na si dhambi tu, bali magonjwa. Kumbukeni, Yesu alisema, "Kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka wa shaba, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa." Musa aliiinua kwa sababu gani? Kwa ajili ya dhambi, kutokuamini, na kwa ajili ya magonjwa. Yesu aliiinuliwa, pia, kwa ajili ya dhambi, magonjwa, na kutokuamini. Yeye alikuwa ni kitu kile kile.

46 Sasa, usiku wa leo, katika siku ambazo tulipata hitilafu hii kuu, Yesu Kristo aliahidi katika Luka, ya kwamba katika siku za ... kabla ya kule Kuja kwa Bwana, ingekuwa kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, na wakati Mwana wa mwanadamu angejifunua Mwenyewe, kama vile Mwana wa Adamu alivyojifunua kwa Ibrahim kule chini; Elohimu, Mungu, aliyefanyika mwili mionganoni mwa watu, na akakaa pale pamoja na Ibrahim na kumwonyesha, akamwambia yale Sara aliyokuwa akiwazia (ameketi nyuma Yake) hemani, ambayo hakuwa amewahi kuona. Akamwambia yale yeye ... Naye akamwita jina lake, "Sara." "Ibrahim," si—si jina lake Abram, aliloanza nalo, bali Ibrahim. Si Sarai, S-a-r-a-i; lakini S-a-r-a, "Yuko wapi mkeo, Sara?"

Kasema, "Yumo hemani nyuma Yako."

Kasema, "Nitakuzuru kulingana na wakati huu wa mwakani." Naye akachecha. Akasema, "Kwa nini alicheka?"

Sasa, Yesu alisema, "Kabla tu ya kukusanya na kuteketezwa kwa hitilafu hii kubwa, kwamba Mwana wa Adamu atajifunua Mwenyewe katika jinsi ile ile kama alivyojifunua wakati huo." Na hiyo ni ... Ni kitu gani? Ni kuinuliwa, upya, mbele zenu, ya kwamba Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Mnaamini jambo hilo? Hebu na tuinamishe vichwa vyetu basi kwa maombi.

47 Mungu mpendwa, tunakupenda. Neno Lako ni mlo m—mkubwa sana kwetu, Bwana. Tunalipenda tu! Tunaishi kwalo, Bwana. Inaonekana kwamba uwezo wetu kamwe hautoshi. Tunapenda tu kuketi kwenye meza Yako, kuzunguka Neno Lako, na kufurahia baraka, Bwana, tunapokusanyika pamoja namna hii, ndugu na dada ambao wamenunuliwa kwa Damu na Mwana wa Mungu, ambao ni ununuzi wa Damu Yako. Nasi tunakuja hapa usiku wa leo, Bwana, tumeziweka wakfu siku hizi za usiku kwa ajili ya kuwaombea wagonjwa. Na kulingana na Maandiko, Wewe ulisema ya kwamba "kwa mapigo sisi tuliponywa." Kwa hiyo si lazima kuomba basi (ni kutubu tu dhambi zetu), kwa maana kwa mapigo Yako tuli-(wakati uliopita)-ponywa. Loo, ni siku ya wokovu iliyoje! Ni ni—ni ahadi iliyoje ya Imanueli! Kwamba hakika ni Kweli.

Wewe ulisema, "Kitambo kidogo, na ulimwengu hautaniona Mimi tena, bali ninyi mtaniona, kwa kuwa Mimi" (kiwakilishi nomino cha "Mimi") "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Na kwenye ukamilifu wa dahari, ukamilifu huu mkuu wa dahari, Wewe ulisema, kabla tu jambo hilo halijatukia, itakuwa tu kama ilivyokuwa kabla ya moto kushuka Sodoma na kuuteketeza ulimwengu wa Mataifa, ya kwamba kungetokea tena kufunuliwa kwa Mwana wa Adamu kama tu vile ilivyokuwa kule Sodoma. Baba, jalia watu wasilikose.

48 Nami ninaomba, Mungu, kama kitu kidogo ovyoovyo, (kama nilisema vibaya, nisamehe), kuweka gia. Ninawapenda, Bwana. Ni—ninaomba ya kwamba hawatalikosa. Jalia huu uwe mmoja wa zile siku kuu za usiku, Bwana. Jalia kila mgonjwa, anayeteseka, kipofu, cho chote kilicho hapa, Bwana, aponywe usiku wa leo. Jalia kila mwenye dhambi aokolewe. Moja kwa moja miyoni mwao sasa, kama wao ni wasioamini, na jalia wamkulabali Kristo wakati huu. Tujalie, Baba. Yote yako mikononi Mwako. Tunajikabidhi Kwako, kukuona Wewe ukija mionganii mwetu.

Nawe ulisema, katika Yohana Mtakatifu 14:12, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya." Jinsi tunavyojua ya kwamba ulijitambulisha kwa watu, kwa kuwa Wewe ulikuwa yule Nabii ambaye Musa alisema angeinuka. Hawakuwa na manabii kwa mamia ya miaka, hitilafu ilikuwa kila mahali, lakini hata hivyo ilibidi Neno la Mungu litimizwe; kwa hiyo Neno likawa mwili, na vivyo hivyo hitilafu. Na, Baba, tunaona jambo hilo tena leo, hitilafu ikifanywa kuwa tita moja kubwa mno; nasi tunaona Neno likija vivyo hivyo. Tubariki usiku wa leo, Baba. Tunajikabidhi Kwako, pamoja na Neno Lako. Lo lote unalohitaji tufanye, fanya nasi, Bwana. Katika Jina la Yesu. Amina.

49 [Dada fulani ananena kwa lugha nyingine. Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.] Hatujui alichosema. Huenda akawa anataka kutwambia jambo fulani, kwa hiyo iweni na kicho sana kwa muda kidogo tu. [Sehemu tupu kwenye kanda. Ndugu fulani anafasiri — Mh.]

Amina. Ulipata kusoma [Sehemu tupu kwenye kanda — Mh.] Maandiko ambapo adui alikuwa akija, nao wote walikuwa wamekusanyika pamoja, nao ... adui alikuwa na nguvu kubwa sana. Ndipo Roho wa Mungu akashuka juu ya mtu fulani, na kumwambia, naye akatabiri, na kusema mahali watakapoenda na kuwavizia, nao wakamwangamiza adui wao. Huyo hapo anakuja tena. Hapo ndipo mahali pa kumwangamiza adui yako, mnaona, chukua mkono wa Mungu. Mkono wa Mungu ni Kristo, bila shaka, Neno, kwa hiyo chukueni Hilo miyoni mwenu usiku wa leo tunapoita mstari wa maombi.

50 Ninaamini Billy alitoa kadi za maombi tena leo. B, B, hebu tuchukue B, themanini na tano. Jana usiku, tulikuwa na kumi na watano jana usiku. Kwa kawaida tunajaribu kupata kama kumi na tano kwa usiku. Halafu basi shikeni kadi zenu, tutazipata, sasa. Hebu na tujaribu yapata kumi na tano. Themanini na tano. B, kama Branham, mwajua. B, themanini na tano hadi mia moja. Nasi tunaninii ... Hebu tuone, ni nani aliye na B, themanini na tano, inua mkono wako. Una hakika ... Loo, huko nyuma, vema, themanini na tano wanakuja.

Sasa, mwanangu ... Kwa hiyo huenda kukawa na wageni hapa, wasingejua namna jambo hili lilitiyofanywa. Mwanangu huja huku, ama mtu fulani; kama hataweza kuja, Ndugu Borders, mtu mwengine. Mtu fulani atakuja hapa, na kuzichukua kadi hizi, mia moja ya hizo, kisha akiwa anasimama mbele za watu na kuzichanganya pamoja. Kwa hiyo basi anakupa kadi, hawezi kukwambia utapanda hapa jukwaani, yeye hajui hilo. Na wala mimi sijui. Ninakuja usiku, ninachukua tu kama kumi ama kumi na tano, mahali fulani hapo, katika hizo kadi. Hilo halina uhusiano wo wote na uponyaji wako. Unaweza kuketi papo hapo. Angalia, jana usiku. Ni wangapi waliokuwa hapa jana usiku, hebu tuone mkono wako? Jinsi watu walivyoponywa tu kote mkutanoni!

51 Sasa, hiyo ilikuwa ni themanini na tano, themanini na sita, themanini na saba, themanini na nane, themanini na tisa, tisini. Hebu na waje sasa hivi. B, themanini na tano, themanini na sita, themanini na saba, themanini na nane, themanini na tisa, tisini. Huyo angekuwa ni mmoja ... Hakika, tunahitaji ... Na kama mtu fulani ... Huyu hapa mwengine, naam, hiyo ingelifanya hilo kutimia. Tisini, tisini hadi mia moja sasa. Tisini, tisini na moja, tisini na mbili, tisini na tatu, tisini na nne, tisini na tano, tisini na sita, tisini na saba, tisini na nane, tisa.

Kama huwezi kusogea, kama wewe ... Ninaona tuna jozi, viti vitatu vya magurudumu hapa sasa, vinne, naamini, ninaweza kuona. Kama una kadi ya maombi, kwamba—kwamba namba yako imeitwa, wala huwezi kusogea, inua tu mkono wako, tutakisukuma mpaka hapa.

52 Na kama huna kadi ya maombi, keti tu pale na uombe, na useme, "Bwana Yesu, hebu—hebu—hebu iwe mimi usiku wa leo." Ni wangapi humu ndani wasio na kadi ya maombi, inua mkono wako. Loo, jaman! Vema, sasa hebu tuseme tu jambo hili, natumaini halisikiki la kukufuru. Lakini kuna maskini mwanamke mmoja wakati mmoja ambaye hakuwa na kadi ya maombi, tungenesema. Alienda akijipenyeza kwenye umati wa watu, akasema (sasa sikilizeni kwa makini), "Kama ninaweza kugusa mavazi ya Mtu huyo, nitapona." Ni wangapi wanaojua hadithi hiyo? Vema. Naye alifanya nini? Alimgusa, kisha akaenda pale akaketi. Ndipo Yesu akageuka, Yeye alijua mahali alipokuwa. Hiyo ni kweli? Alijua shida yake ilikuwa ni nini. Hiyo ni kweli? Alijua shida yake ilikuwa ni nini, kwa hiyo akamwambia shida yake ilikuwa ni nini. Naye akahisi mwilini mwake ya kwamba kutokwa na damu kumekoma. Hiyo ni kweli? Kwa sababu ni kwa nini? Alikuwa amemgusa.

53 Sasa, ni Wakristo wangapi hapa usiku wa leo wanaojua, kulingana na Waembrania, Kitabu cha Waembrania, ya kwamba Yesu sasa hivi ni Kuhani Mkuu, Kuhani Mkuu anayeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu? Sivyo? Vema, kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, huduma ile ile, Kuhani Mkuu, Yeye angetenda vipi basi? Yeye angetenda vile vile tu kama alivyatenda wakati huo. Mnaamini

jambo hilo? Yeye angetenda vile vile tu kama alivyofanya wakati huo, kama unaweza kuamini jambo hilo. Vema. Ni wangapi wanaoamini jambo hilo, inua mkono wako, useme, "Kwa kweli ninaamini"?

Vema, kabla hawajafanya mstari wa maombi, hebu na tuwe na mstari wa maombi huko nje. Ninajua Yeye yuko hapa. Na—na—najisikia Uwepo Wake, nami na—najua ya kwamba Yeye yupo hapa. Njoo. Mstari wa maombi uko tayari? Nilikuwa niite kule. Ninyi tu—ombeni tu, angalieni tu huku na kuomba, aminini tu.

54 Bibi mdogo anayeketi hapa akiniangalia moja kwa moja, ameketi karibu na mama aliyevaa miwani. Je! huwezi kuona Hiyo ikining'inia juu ya mwanamke huyo? Angalia hapa. Mnaona? Yeye anaugua ugonjwa wa moyo. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Kama unaamini, inua mkono wako. Hiyo ndiyo iliyokuwa shida yako. Hiyo ni kweli. Sasa kama hiyo ilikuwa shida yako, inua mkono wako ili watu waweze kuona, inua mkono wako namna hiyo. Sasa, huna huo tena. Imani yako imekuponya.

Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Loo, kuna hitilafu; bali Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Je! ni hii ... Sasa endeleeni tu kuomba, mnaona, si lazima uwe hapa juu, upate kujua.

55 Sasa, huyu ni mama. Nijuavyo mimi, sijapata kumwona maishani mwangu, yeye ni mwanamke tu anayesimama hapa, na ana kadi ya maombi, wala hukujua kama utaitwa au la. Mtu fulani anakupa tu kadi ya maombi, nawe—nambari yako inaitwa, kwa hiyo uje tu hapa. Hiyo ni kweli? Nami sina njia ya kujua wewe ni nani, wewe ni nani, unakotoka, unachotaka, sina kitu juu yake. Mimi ni mwanamume tu, wewe ni mwanamke. Hiyo ni kweli. Picha hii hii ilikuja wakati mmoja katika Biblia, Yohana Mtakatifu, mlango wa 4.

Sasa unasema, "Ulifanya nini, Ndugu Branham, wakati huo tu, muda mfupi uliopita?" Nilivuta tu gia hiyo ndogo, mnaona. Sijui, mnaona. Hana budi kufanya hivyo. Sijui. Huyo mwanamke huko nje alifanyaje? Sijapata kumwona mwanamke huyo maishani mwangu. Yeye ni mgeni kabisa kwangu. Ninaamini ilikuwa ni mwanamke. Ni nani mtu aliyeponya sasa hivi nje katika wasikilizaji? Utaninii ... Naam. Sisi hatufahamiani. Kama hiyo ni kweli, punga mkono wako namna hii. Mnaona? Sijapata kumwona mwanamke huyo. Lakini alikuwa ameketi pale, akiamini. Sasa, yeye aligusa kitu Fulani, sivyo? Haingefaa kitu kunigusa mimi.

56 Lakini sasa huwezi kuona ya kwamba Biblia ni Neno la Mungu hasa? Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Tunakuwa maskani ya huyo Roho Mtakatifu ambaye ni Kristo. Mnaona? Hiyo ndiyo Mbega halisi. Basi kama huyo Roho Mtakatifu halisi akiingia katika Mbega halisi ya Neno, si ... Hiyo haitachukua sehemu Yake tu (kwa sababu, Ibilisi anatumia Hilo), huna budi kuchukua yote, unaona, kila Neno Lake; maana, Yeye si Mungu nusu, ni Mungu kabisa. Mnaona? Na hilo ndilo linalotukia.

Sasa, huyu hapa mwanamke, sijapata kumwona. Yesu alimkuta mwanamke kama huyu wakati mmoja, labda si hali ile ile, sijui. Naye alikuwa ameketi kisimani. Yeye—Yeye alikuwa na haja ya kushuka kwenda Samaria. Nasi tunaona, Samaria ilikuwa chini ya kilima. Na—naye alikuwa akienda Yeriko, hasa, Naye alizunguka karibu na Samaria, na akaja kwenye mji wa Sikari. Ndipo Yeye akaketi chini pale kisimani, akawatuma wanafunzi Wake waende wakanunue chakula.

57 Kuna jamii ngapi za watu ulimwenguni? Tatatu. Watu wa Hamu, Shemu, na Yafethi. Sote tunatoka kwa Nuhu. Nao ulimwengu uliosalia uliangamizwa wakati huo. Ni jamii tatatu za watu, yule Myahudi, Mmataifa, na Msamaria (ambaye alikuwa nusu Myahudi na Mmataifa). Na hizo ndizo jamii zote zilizo ulimwenguni, mnaona, tatatu tu.

Kila kitu katika Mungu ni kikamilifu katika utatu. Ni kama tu vile hivi vitatu nilivyokuwa nikizungumzia usiku wa leo: hatua tatu za hitilafu, hatua tatu za Neno lililofanyika mwili, na kadhalika. Mnaona?

Sasa, na Yeye—Yeye aliyezungumza na Wayahudi, alimwambia Filipo, wakati alipomleta Nathanaeli, mahali pale alipokuwa, na kusema, "Nilimwona wakati alipokuwa chini ya mtini." Andrea alikuwa amemleta Petro, Yeye akasema, "Jina lako ni Simoni, nawe utaitwa 'Petro' tangu sasa na kuendelea." Kasema, "Wewe ni mwana wa Yona." Mnaona? Sasa, hao wote walikuwa ni Wayahudi.

Lakini hapa anaenda kwa Mmataifa ... si Mmataifa, bali Msamaria.

Sasa huu ndio wakati wa Mataifa. Yeye kamwe hakufanya jambo hilo kwa wakati mmoja kwa Mataifa. Yachunguzeni Maandiko. Kamwe. Lakini Yeye aliahidi, katika Luka 22, ya kwamba angefanya jambo hilo kabla tu ya kule Kuja.

Lakini Yeye aliketi kule chini, na huyu hapa nusu Myahudi na Mmataifa, mwanamke. Naye akamwambia, "Mwanamke, nipe maji ninywe."

Akasema, "Mbona, hupaswi kuuliza jambo hilo, sana. Sisi ni ... Kuna ubaguzi hapa. Wewe ni Myahudi, na—nami ni Msamaria."

Yeye alisema, "Lakini kama ungalijua ni Nani unayezungumza naye, ungeniomba Mimi maji." Alikuwa

akifanya nini? Akiwasiliana na roho yake. Na mara alipopata shida yake ilikuwa ni nini, vema, Yeye alimwambia aende akamlete mumewe. Akasema hakuwa na ye yote. Akasema, "Hiyo ni kweli, umekuwa na watano."

58 Sasa, angalia, wakati Mafarisayo walipomwona akifanya jambo hilo. Vema, hiyo hitilafu moja kwa moja mionganoni mwa Neno, walisema nini? Wao walisema, "Mtu huyu ni Beelzebuli, mpiga ramli." Mnaona?

Naye Yesu alisema, "Ye yote aliyesema hayo juu ya Roho Mtakatifu atakapokuja kufanya jambo lile lile, hatasamehewa kamwe." Hiyo hapo hitilafu yako. Mnaona? Lakini Yeye alisema angewasamehe wakati huo, kwa sababu Roho Mtakatifu hakuwa amekuja; ile Dhabihu, Mwana-Kondoo hakuwa amekufa.

Lakini basi mwanamke huyo hakufikiria jambo hilo. Yule mwanamke akasema, "Bwana, naona ya kwamba Wewe ni nabii." Hawakuwa na nabii kwa mamia ya miaka. Kasema, "Ninaona Wewe ni nabii. Sasa, tunajua ya kwamba Masihi, ambaye anaitwa Kristo, wakati atakapokuja, hilo ndilo atakalofanya."

Vema, kama hivyo ndivyo alivyofanya, basi ni yeye yule jana, leo. Hivyo ndivyo alivyoitambulisha wakati huo, si ni jambo lile lile leo? Haina budi kuwa! Sasa, huyu hapa mwanamke na mwanamume wanakutana tena. Yeye si mwanamke huyo, mimi si Mwanamume huyo. Lakini hata hivyo Roho Mtakatifu yeye yule yuko hapa, naye aliahidi ya kwamba kazi alizozifanya, tungefanya mambo yayo hayo katika siku za kufunuliwa kwa Mwana wa Adamu.

59 Sasa, bila kukuja (na unajua hiyo ni kweli), sisi ni wageni kabisa, nawe umesimama hapa. Kuna baadhi ya ... Huenda kukawa na kasoro, labda hakuna, sijui. Lakini kama Bwana Yesu atanifunulia, kwa Roho Wake Mtakatifu, shida yako ni nini, utaamini basi ya kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu, wala si mwanadamu? Hili ni ganda tu, maskani hii ambayo—ambayo Mungu anatumia, ye yote ambaye Yeye amemchagua. Yeye—Yeye hufanya hivyo kwa neema kuu na kuchaguliwa. Kwa hiyo, lakini unaamini. Utafanya hivyo? [Mwanamke huyo anasema, "Amina"—Mh.]

Ni wangapi katika wasikilizaji watakaoamini jambo hilo? Hapa sisi sote wawili tunasimama papa hapa mbele ya ile Nuru, ya kwamba hatujawahi kukutana katika maisha haya, hatujui tena mwanamke huyo ni nani, ni nani, anakotoka, anachotaka. Sijapata kumwona maishani mwangu, si zaidi ya nilivyopata kumwona mwanamke yule pale chini maishani mwangu. Lakini, unaona, hivi ndivyo ninavyojaribu kuwafanya mfanye: ondooleeni mbali hiyo hitalafu, na mwamini Neno wakati Neno linapofanyika mwili papa hapa kati yetu. Neno linakuwa hai katika miili yetu wenyewe, hilo linaonyesha Uwepo wa Mungu.

60 Sasa na amjalie. Yeye anataka jambo linalostahili. Yeye hana mtoto, anataka mtoto mchanga. Yeye ana umri wa kama miaka arobaini. Hilo hakika si jambo lisilowezekana.

Wanaketi papo hapo nje sasa, wanawake waliokuwa tasa maishani mwao mwote, na wakaja jukwaani namna hii, na Bwana akawapa watoto. Wengine wenu inua mkono wako huko nje wanaojua. Mnaona? Mnaona? Nilimchukua msichana mdogo mpendwa hivi majuzi, Jumapili, baada ya mimi kuondoka hapa, Jumapili alasiri; ya kwamba mama yake alikuwa tasa, Bwana alinena. Na huyo msichana mdogo, kitu kidogo kitamu sana, yupo hapa? Yuko wapi? Naam. Huyu hapa, papa hapa, ameketi papa hapa chini. Yule mama anayeketi pale. Huyu hapa yule msichana mdogo, yeye mwenyewe. Mnamwona? Alikuwa ni Neno lililonenwa kutoka kwa Mungu.

Sasa, je! Utamwamini Yeye kwa moyo wako wote? Je! Unaamini ya kwamba ile baraka uliyo nayo, ambayo unajisikia ndani yako sasa, imekuwa ni Mungu akijibu? Kama Mungu angeniambia jina lako ni nani, ili uweze kumpa mtoto huyo jina, ungeamini? Halafu, Bibi Thompson, unaweza kwenda nyumbani ukampate mtoto wako, kama utaamini kwa moyo wako wote.

61 Je! Unaamini kwa moyo wako wote? Iweni tu na imani, msitie shaka, mwamini tu Mungu. Mungu ni Mungu.

U hali gani, bwana? Nadhani sisi ni wageni, pia. Wakati pekee niliopata kukuona maishani mwangu, nijuavyo mimi, ni wakati ulipokuwa ukija kule. Nami nilifikiri wewe ulikuwa ni mjomba wa Ndugu Shakarian, ama ni nani ... Mashagian, Ndugu Mashagian, yule mwimbaji, ulipopitia hapa. Na halafu nikaona mlikuwa mnaenda kwenye mstari wa maombi. Sasa, nikiwa mgeni kwako, na, ama kwako, nami nikiwa mgeni, vyo vyote vile. Sasa, kama Bwana Yesu ataniamibia jambo fulani ambalo umeninii—jinsi ulivyo, kile unachohitaji, hebu na tuseme hivyo tu; akwambie nini, aniambie unachotaka. Sasa, Yeye tayari amekupa. Jambo pekee ni imani ya kutosha tu kuliamini.

Sasa, ni wangapi wanaofahamu jambo hilo? Ni imani ya kutosha tu kuamini ya kwamba unapata kile unachoomba! Mnaona?

62 Sasa, sasa, kama uko juu hapa unataka kitu fulani, Naye anaweza kuniambia shauku yako ni nini, basi unajua sijui haja yako, basi haina budi kuwa na Kitu fulani hapa kinachofanya jambo hilo. Sasa, kulingana na Neno, Yeye aliahidi kufanya hivyo. Yeye alijua mawazo ndani ya mioyo yao. Hiyo ni kweli? Vema.

Una shaku kubwa ya kuponywa. Jambo moja, unaugua ugonjwa wa neva, wasiwasi sana. Hiyo ni kweli. Jambo lingine, una ugonjwa wa mgongo, na mgongo huo umekuwa mbaya sana kwa muda fulani, hata umefanyiwa upasuaji. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Hiyo ni kweli. Mnaona. Hiyo ni kweli. Na hapa kuna jambo lingine, shaku yako ya kina, ni, unataka kupokea ubatizo wa Roho. Hiyo ni kweli kabisa. Njoo hapa.

Mungu mpendwa, katika Jina la Yesu Kristo, mtu huyu na ajazwe na Roho Mtakatifu, kabla hajaondoka kwenye misingi hii, katika Jina la Yesu. Amina.

Sasa lipokee, ndugu yangu. Iweni tu na imani, msitie shaka.

63 U hali gani? Nadhani, kadiri niujuavyo mimi, ya kwamba sisi hatufahamiani. Kama hiyo ni kweli, mbona, ili kwamba watu wajue, inua tu mkono wako kusudi waone ya kwamba sisi ni wageni. Sijapata kumwona maishani mwangu, kwa kujua. Nami nadhani yeye hakuwahi kuniona kamwe, isipokuwa iwe ni huko kwa wasikilizaji. Kwa sababu Baba wa Mbinguni anajua, na hili hapa Neno Lake liko hapa, ya kwamba sijapata kumwona mwanamke huyu, kwa kujua, maishani mwangu. Kwa hiyo, nisingejua kilichokuleta hapa, sijui wewe ni nani, nini, wala chochote kukuhusu. Nisingewenza kuwaambia jambo moja.

Jambo pekee, ni karama tu. Kama ninaweza ... Kama mlivyonisikia nikielezea jambo hilo muda mfupi uliopita. Nenda tu huku, usikie yale anayosema; yale ninayoona, naweza kuyasema. Yale asiyosema, siwezi kuyasema. Ningesema hilo ndani yangu, na ingekuwa ni kosa. Mnaona? Ingekuwa ni kosa. Lakini kama akisema jambo hilo, ni kweli kabisa. Haiwezi kamwe, kamwe halijapata kuwa makosa. Kamwe halitakuwa makosa mradi tu inadumu kuwa ni Mungu. Mnaona? Mnaona, kwa sababu Mungu hawezikukosea.

64 Lakini kama Mungu anaweza kuniambia unachotaka, shaku yako ni nini, ama—ama kilichokuleta hapa, jambo fulani ambalo umefanya, ama cho chote kile, kitu kama hicho, ama kwamba wewe ni nani, unatoka wapi, ama cho chote anachotaka kuniambia, ungweza kuamini? Asanteni.

Jambo moja, una shida kwa miguu yako. Miguu yako inakusumbua. [Mwanamke huyo anasema, "Ndiyo"- Mh.] Hiyo ni kweli. Inua ... Una shida ya mwanamke, ugonjwa wa kike. ["Ndiyo."] Na una shaku kuu moyoni mwako, kwa sababu umempoteza mtu fulani ama kitu fulani. Ni mvulana, na mvulana wako ameondoka nyumbani, amekimbia, nawe unataka niombe ya kwamba atarudi. ["Ndiyo."]

Mungu Mbinguni, mtume mtoto wake, na uponyaji. Jalia Roho Mtakatifu amzuie huyo kijana njiani usiku wa leo, amrudishe kwa mama yake. Katika Jina la Yesu. Amina.

Yeye anayejua atamrudisha kwako. Usijali. Amini sasa, usitie shaka. Iweni tu na imani, moyo wenu wote. Unaamini, na Mungu atakujalia hayo mengine.

65 Sasa, pambanuzi hizo tatu au nne, cho chote kile, unaona, ni—nilienda tu mpaka nikawa sioni. Siwezi kuelezea jambo hilo, hakuna njia ya kulielezea. Unasema, "Unamaanisha, hilo tu lilikuwa baya kuliko ulivyohubiri pale kwa dakika arobaini na tano ama zaidi, unafikiri?" Naam, bwana. Kama ingekuwa ni saa tatu, isingekuwa kiasi hicho.

Mwanamke mmoja aligusa vazi la Bwana wetu Yesu. Na hao watu hawanigusi. Mbona, mwanamke huyu hapa, angalia tu hapa, angeweza ... [Ndugu Branham anamwambia mwanamke huyo, "Weka mikono yako juu yangu, unaona." - Mh.] Yeye alinigusa tu kila mahali, asingeweza kufanya jambo lolote, mimi ni mwanamume tu. Bali hana budi kumgusa. Nami, kwa karama, ninii tu—tu ... inaondoka tu, nafsi yangu yote inaondoka, nami ninasema tu yale ninayoona. Mnaona? Na hivyo tu. Mnaona, kunigusa mimi hakumaanishi kitu, bali anamgusa Yesu kuititia kwangu. Hivyo ndivyo mwanamke huyo alivyomgusa Mungu kuititia kwa Yesu, wakati Yeye hakuja alikuwa na shida gani. Aligusa tu vazi Lake, akaenda akaketi. Naye akasema—naye akasema, "Ni nani aliyenigusa?"

Nao mitume wakasema, "Mbona, kila mtu anakugusa. Kwa nini unasema hivyo?"

Yeye alisema, "Lakini ninaona ya kwamba nguvu zimenitoka."

Sasa, unajua nguvu ni nini? Nguvu. Alidhoofika kwa mwanamke mmoja kumgusa, Naye alikuwa Mwana wa Mungu. Vipi kuhusu mimi, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema Yake. Unajua ni kwa nini ni zaidi? Kwa sababu Yeye alisema, "Mambo haya nifanyayo, ninyi nanyi mtayafanya pia. Zaidi ya haya mtafanya, kwa kuwa Mimi naenda kwa Baba Yangu." "Kubwa zaidi," lilisema pale, bali tafsiri sahihi ya Kiyunani ni, "Zaidi ya hizi mtafanya."

66 Sasa, mama huyo simjui. Sijui lolote kumhusu. Yeye ni mgeni kabisa kwangu kama watu wengine walivyokuwa. Sisi hatufahamiani. Ili tu kwamba watu wajue jambo hilo, unaweza kuinua mkono wako, useme "sisi ni wageni." Sasa, Mwana wa Mungu, kama wakati mmoja alikutana na mwanamke katika mandhari ndogo kama hii, karibu na kisima, Naye akazungumza naye kwa muda kidogo tu, Naye alijua shida yake ilikuwa wapi, Naye akamwambia shida yake ilikuwa ni nini? . Na kwa hiyo alijua kwa jambo hilo,

ya kwamba huyo alikuwa ni Masihi. Sasa kwa kuwa—kwamba nime ... Umenigusa, nimekugusa, wala hakuna kitu kilichotukia. Lakini kama imani yangu (kwa karama fulani) na imani yako (kwa kuiamini) naweza kumgusa Yeye, Naye anaweza kunena kupitia kwetu kuninii...kwako kupitia kwangu, ndipo unajua ya kwamba Yeye yuko hapa kama alivyokuwa kwenye kile—kile kisima Sikari. Mnaona? Ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Unaamini jambo hilo?

Una shida nyingi sana, mateso mengi sana, matatizo! Moja ya mambo makuu unayotaka kuombewa ni yabisi kavu. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli? Unakakamaa kwa yabisi kavu. Unapoona ukiinua mkono wako ...

67 Nawe ulitembea polepole, vizuri sana nikikumbuka. Labda ngoja kidogo tu, labda jambo lingine linaweza kusemwa ambalo litachukua ... Ama, unajua, unajisikia mambo; watu, mwajua, kama pumzi ikija dhidi Yake. Wanasema, "Mbona, alibashiri jambo hilo," ama, mwajua, namna hiyo.

Lakini, unaonekana wewe ni mtu mzuri, nizungumzie tu kwa muda kidogo. Hebu na tusimame hapa kidogo, kwa sababu nafikiri kuna kitu kingine ambacho kiko moyoni mwako ambacho unataka kutoka kwa Mungu. Sasa, nisingeweza kujibu ombi lako, bali Yeye anaweza kuninii ... Kwa sababu, kama unaamini, tayari limejibowi. Lakini kama unataka tu kuamini; kukufanya uamini. Sasa, nawaambia, ni kuhusu mpendwa ambaye hayupo hapa, na huyo ni ndugu, na ndugu huyo hata hayuko katika nchi hii. Yeye yuko katika nchi yenye mvua, maziwa mengi. Ningesema kama kitu kama vile Michigan ama ... Naam, Michigan ndipo alipo. Naye anaugua ugonjwa wa kuua, na huo ni ugonjwa wa figo usiopona ambao unamsumbuwa. Hiyo ni kweli, sivyo? Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Sasa, leso uliyo nayo mkononi mwako, uliyomwinulia Mungu, tuma hiyo kwa ndugu yako na umwambie asitilie shaka, bali aamini, na hiyo itakuwa, ataponywa sasa kama utaamini .

68 Unaamini kwa moyo wako wote? Mnaona, basi, kama unaamini, kuna jambo moja tu la kufanya, hilo ni, likubali kabisa. Hiyo ni kweli?

Sasa unasema, "Yeye anaangalia jambo hilo, hao watu. Hivyo ndivyo anavyofanya, akiwaangalia." Mnaona jambo hilo sana!

Lakini ili kwamba msijue jambo hili ... Bibi huyu hapa, njoo huku, bibi, hapa, mgonjwa, ye yote uliye. Simwangalii. Je! Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kunifunulia shida yako? Inueni mikono yenu, kama mkifanya hivyo, mama huyu hapa, mama huyu hapa, mgonjwa. Naam. Naam. Vema, basi kama utaamini hilo kwa moyo wako wote, ugonjwa huo wa pumu hautakusumbua tena. Vema, nenda nyumbani ukaamini.

69 Sikumwangalia, sivyo? Mnaona, Yeye ... Unaangalia upande huu, ono liko pale haidhuru ni jambo gani linalotukia. Amina! Hamwezi kuliona? Kamilifu kabisa kama vile Mungu anavyoweza kuwa mkamilifu!

Unaamini, pia? Pumu inaweza kukuacha, pia, sivyo? Unaamini ingekuwa hivyo? Vema, nenda ukamwambie Bwana Yesu ya kwamba u—unamwamini.

Siku moja itakubidi kubeba fimbo ndo—ndogo ukienda huku na huko kama hiyo yabisi kavu ikitikulemaza, lakini haitakulemaza. Huwezi, huamini ndivyo ilivyo, sivyo? Unaamini utakuwa mzima? Nenda zako, na Yesu Kristo anakuponya.

Ugonjwa wa moyo huua watu, bali si lazima ukuue. Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya, na kukupa afya? Nenda ukiamini kwa moyo wako wote, useme, "Ninaamini kweli kwa ajili yake."

70 Mnazungumza Kiingereza? Mnaelewa Kiingereza? [Ndugu Branham anaomba mfasiri — Mh.] (Mtu fulani na aje.) Naam, sawa. Utamwambia yale nitakayomwambia? Mwambie kama ataamini, ugonjwa wa tumbo utamwacha. Yeye—yeye ataamini jambo hilo? Ugonjwa wako wa mgongo utakuacha, pia, kwa hiyo sasa unaweza kwenda zako na kuponywa.

U hali gani? Unaamini? [Yeye unasema, "Naam, bwana." - Mh.]

Mtu huyo anayeketi pale mwenye ugonjwa wa mgongo, akiniangalia niliposema jambo hilo. Anaweza kuponywa, pia, kama unaamini, bwana. Vema, bwana.

Bibi anayeketi papo hapo karibu nawe pale, una shida ya shingo, sivyo, bibi? Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Unataka kuweka mikono juu ya mvulana huyo mdogo kwa ajili ya magoti yake, naye atapona, pia. Mnaamini jambo hilo? Ulikuwa na shida ya kike, shida ya mama, huna hiyo sasa. Imani yako ilikuponya na kukufanya mzima.

71 Unamwamini Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele? Basi hebu na tuwekeane mikono na kuomba dua hili la imani, kila mmoja wetu, tuombe maombi ya imani.

Mungu mpandwa, wakati tumefunikwa sana katika Uwepo Wako wa Kiungu, kukuona ukitembea kupitia kwa wasikilizaji, ukiponya wagonjwa kila mahali. Wewe ni Mungu. Ninaomba ya kwamba utawaponya wasikilizaji hawa wote. Jalia Pumzi ya Mungu ishuke upya ndani ya miyo yao, na jalia wao

wajue ya kwamba wakati unakwisha. Tuko na muda kidogo tu zaidi kuwa hapa, ndipo tutakuwa pamoja na Yeye tunayempenda. Na jalia sasa Uwepo Wake ulete uponyaji kwa kila mtu.

Tunamhukumu Shetani, tunalaani matendo yake yote. Katika Jina la Yesu Kristo, Shetani, toka kwa watu.

Wote watakaomwamini Yeye sasa, na mnakubali uponyaji wenu, simameni kwa miguu yenu, semenii, "Sasa ninasimama kukubali uponyaji wangu. Ninaamini jambo hilo." Haidhuru una hali gani, kama kweli unaamini jambo hilo, simama kwa miguu yako. Sasa inua mikono yako, na useme, "Asante, Bwana Yesu, kwa kuniponya." Mungu awe pamoja nanyi.



www.messagehub.info

Mahubiri Na

William Marrion Branham

"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7